YANTAQIDŪN WA YUNKIRŪN AT-TAHAZZUB WA'L-HIZBIYYAH WA HUM MUTAHAZZIBŪN!!

WAO WANAKOSOA NA KUPINGA TAHAZZUB NA HIZBIYYAH, HALIYAKUWA WAO WENYEWE NDIWO MUTAHAZZIB [POTE]

Sheikh Sâlim at-Twawîl
Tarehe 7 Muharram 1435 AH/2 November 2014 CE, Tizama katika:
http://www.saltaweel.com/articles/368
Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad

Kila sifa njema zinamstahiki Allâh, hakuna uadui isipokuwa kwa mwenye kudhulumu na mwisho mwema ni kwa watu walio wema, na swala na salamu zimfikie Mtume wetu, na ahli zake na Maswahaba zake wote, Amma baada ya hayo:

Ta'assub na *Tahazzub* ni maradhi yenye uvundo kama ambavyo Mtume (ﷺ) alivyosema: *"Uacheni kwani (huo) ni uvundo."* Imepokewa na al-Bukhâri (No. 4905). Wale wenye kukosoa na kupinga Tahazzub au Hizbiyyah wamejitokeza na wanaonyesha ukali dhidi ya ma-Hizbi. Wao hufikilia mpaka kupigana, wakawafanyia *tabdî'* au kukatana nao, hata wakaonyesha uadui kwa yoyote ambaye hatowafanyia *tabdî'* au kuonyesha utwiifu juu ya *tabdî'* yao. Kisha mtu kama huyo pamoja na wale alionao anakuwa mfuasi wa kikundi au 'mlokole'[1], Uhizbiyyah huanzia katika hali ya udhaifu, kisha polepole ukazidi kuwa na nguvu mpaka hatimae ukawa umestawi baraa bara.

Huu ni ukweli ambao ma-Hizbi wengi wameshindwa kuukubali na si jambo la kushangaza, kama ilivyo yakwamba si kila mgonjwa atakuwa na uwezo wa kuufahamu ugonjwa wake, kwahivyo kwa mfano maradhi ya unafiki ni maradhi maovu zaidi, lakini juu ya hayo yote, wanafiki hawatambui hayo, kama alivyosema Allâh (سبحانه وتعالى):

فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿﴾ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِنْ لَا يَشْعُرُونَ

[1] Mfuasi sugu wa pote au mzalenzo wa chama

“Nyoyoni mwao mna maradhi, na Allâh amewazidishia maradhi (kwa kuwa kila siku yalikuwa yanaongezeka mambo mengine mengine ya Kiislamu ya kuamini na ya kufanya; na ya kuwaudhi kweli kweli). Basi watakuwa na adhabu iumizayo kwa sababu ya kule kusema kwao uwongo. Na wanapoambiwa: “Msifanye uharibifu ulimwenguni.” Husema: “Sisi ni watengezaji.” Hakika wao ndio waharibuji, lakini hawatambui.”
[al-Baqarah (2): 10-12]

Ni watu wangapi wenye kuzidhania nafsi zao wema ambazo ni zenye kuwashawishi kunako maovu na wakaziamini haliyakuwa hazikuwa ni zenye kustahiki kuaminiwa, lakini akadhania yakwamba [nafsi hiyo] inamuamrisha mema hata kama iko mbali na uongofu. Watu wengi hawatambui ukweli huu: Ni vipi mtu anaweza kuwa ni mlinganizi wa makundi na akakosolewa kwa kuwa na Uhizbiyyah, haliyakuwa yeye anaupiga vita na kuwafanyia *tabdî’* wenye huo Uhizbiyyah, kwani kumbe mimi sijui hayo!!! Ni kitu gani chenye kutulinda na hayo? Kulingana na Sheriya ya Dini, busara au mila yenye kumfanya mtu akatumbukia ndani ya jambo ambalo yeye anawatahadharisha nalo watu. Twakuletea baadhi za dalili zenye kuashiriya ninayoyasema:

MOJA:

Allâh (سبحانه وتعالى) amesema:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا ثُمَّ آمَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا ثُمَّ ازْدَادُوا كُفْرًا لَمْ يَكُنِ اللَّهُ لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ سَبِيلًا

“Hakika wale walioamini, kisha wakakufuru, kisha wakaamini kisha wakakufuru, tena wakazidi ukafiri, Allâh hatawasamehe wala hatawaongoza njia (ya kheri).”
[an-Nisâ’ (4):137]

Na akasema Allâh:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ ثُمَّ ازْدَادُوا كُفْرًا لَنْ تُقْبَلَ تَوْبَتُهُمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الضَّالُّونَ

“Hakika wale waliokufuru baada ya kuamini kwao, kisha wakazidi kukufuru; toba yao haitokubaliwa (kamwe), na hao ndio waliopotea (kweli kweli).”
[Âl ‘Imrân (3):90]

Kwahiyo, pana uwezekano kwa kila mtu kuamini, kisha akakufuru, kisha akaamini tena, kisha akakufuru, kisha tena akazidi katika kukufuru. Kwahivyo inachukuwa kipa-umbele yakwamba mtu anaweza kuwacha Tahazzub, akaipinga kabisa na kuipiga vita na kisha yeye mwenyewe akaja akawa ni mtu wa pote na akazidi katika Uhizbiyyah huo hata kuliko wengine na pengine akapindukia zaidi hata kuliko ule Uhizbiyyah aliokuwa akiukosoa.

MBILI:

Allâh (سبحانه وتعالى) Amewakemea kwa kubaki milele katika moto wa Jahannam, watu wenye kuiwacha Dini yao, akasema:

وَمَنْ يَرْتَدِدْ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَيَمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُولَئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

"Na watakaotoka katika Dini yao katika nyinyi, kisha wakafa haliyakuwa makafiri, basi hao ndio ambao amali zao zimeharibika katika dunia na akhera. Nao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele." [al-Baqarah (2): 217]

Kulingana na muafaka wa wanavyuoni, *kuritadi* (kuacha Dini), namuomba Allâh aniepushe mimi na wewe kutokana na uovu huo, kuna hukmu zake maarufu sana zinazojulikana. Baadhi ya waliokuwa wamesilimu katika zama za Mtume (ﷺ) waliritadi (waliwacha Uislamu), kama ilivyopokewa na al-Bukhâri (No.3422) na Muslim (No.2781) kutoka kwa Anas (رضي الله عنه) aliyesema: *"Palikuwa na Mkristo mmoja aliyesilimu, na akawa anasoma katika milango ya al-Baqarah na Âl-'Imrân, na aliwahi kumuandikia* Mtume (ﷺ) . Mara baadae akarudi kwenye dini yake ya Ukristo, na akawa anasema, "Huyu Muhammad hana ajualo isipokuwa yale ninayomuandikia." Kisha Allâh akamja'aliya kufa, na watu wakamzika, lakini asubuhi kulipopambazuka wakaona yakwamba ardhi imeutema mwili wake kutoka kaburini. Wakasema, haya ni matendo ya Muhammad na Maswahaba zake! Wamelichimba kaburi la mtu wetu na wakamtoa mwili wake kutoka kaburini kwa sababu amewakimbia." Wakamchimbia tena kaburi refu zaidi, lakini kulipopambazuka asubuhi wakaona yakwamba ardhi imeutema tena mwili wake kutoka kaburini; wakasema, haya ni matendo ya Muhammad na Maswahaba zake! Wamelichimba kaburi la mtu wetu na wakamtoa mwili wake kutoka kaburini kwa sababu amewakimbia." Wakamchimbia kaburi refu kiasi cha uwezo wao, lakini kulipopambazuka asubuhi wakaona yakwamba ardhi imeutema tena mwili wake kutoka katika kaburi lake. Hapo ndipo walipojua yakwamba yaliyotokea si mambo yaliyofanywa na watu, basi wakamuachilia mbali."

Kweli kuna lolote la zaidi la kuaminika [kuliko hili]? Mimi nasema: Si jambo la kuficha yakwamba mtu anaweza kupotoka baada ya kuongoka, sasa ni kitu gani chenye kumzuiya mtu aliyekuwa ni mkali sana dhidi ya watu wa Hizbiyyah na kuwa Hizbi yeye mwenyewe?!

TATU:

Mara kwa mara Mtume (ﷺ) alikuwa akisema katika maombi yake: *"Ewe Mgeuzi wa nyoyo, uthibitishe moyo wangu juu ya Dini yako."* Imepokewa na at-Tirmidhi (No.3522). Na pindi Mtume (ﷺ) alipokuwa akila kiapo alikuwa akisema: *"Laa, naapa kwa mgeuzi wa nyoyo"*, imepokewa na al-Bukhâri (No.6628). Hii inaashiriya yakwamba mwenye kuupinga Uhizbiyyah anaweza kubadilika na kutumbukia ndani yake yeye mwenyewe, kama ambavyo Muislamu anavyoweza kubadilika na kutumbukia ndani ya ukafiri.

NNE:

Hapa tunae Ibrâhîm, Khalîl wa Allâh (ﷺ), alikuwa akilingania katika Tawhîd, akaukataa ushirikina na kuwavunja masanamu, na alikuwa akisema:

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا وَاجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ الْأَصْنَام

"Na (kumbukeni) aliposema Ibrahimu: 'Mola wangu! Ujaalie mji huu (wa Makkah) uwe wa amani. Na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu."[Ibrâhîm (14):35]

Sasa ni nani aliyesalimika na nafsi yake baada ya Ibrâhîm? Ikiwa aliyeyavunja masanamu alimuomba Allâh amuepushe nafsi yake na watoto wake na kuwaabudu masanamu, basi mbona sisi twajiona tumesalimika na hayo kiasi cha kwamba mlinganizi wa kuumaliza Uhizbiyyah akawa yeye amesalimika na kutumbukia kwenye janga hilo au akapata mitihani kutokamana nao.

TANO:

Allâh amemtaja katika Kitabu chake, Mtume wake Shu'ayb (ﷺ),

وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ إِلَى مَا أَنْهَاكُمْ عَنْهُ

"Wala sipendi kukukhalifuni nikafanya yake ninayokukatazeni…"

Hii inaashiriya yakwamba miongoni mwa watu, kuna wale ambao wanaweza kwenda kinyume cha mambo halisi wanayoyapinga au kuwatahadharisha watu dhidi yake.

SITA:

Allâh (سبحانه وتعالى) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ

"Enyi mlioamini! Mbona (kwa nini) mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Allâh kusema msiyoyatenda." [as-Swâf (61): 2-3]

Hii ni dalili dhahiri inayoashiriya yakwamba pana uwezekano mkubwa yakwamba miongoni mwa watu ni wale wanaoweza kuwatahadharisha watu dhidi ya Tahazzub, haliyakuwa wao wenyewe wakawa ni ma-Hizbi wanaowaka moto!

SABA:

Amepokea Muslim katika swahîh yake (No.2989) kutoka kwa Usâmah Bin Zayd (رضي الله عنه) aliyesema: Nimemsikiya Mtume (ﷺ) akisema; *"Ataletwa mtu katika siku ya Malipo na atavurumizwa motoni. Matumbo yake yatamwagika chini na atakuwa akigaragara na kuyazunguka kama vile anavyozunguka Punda kwenye jiwe la kusaga. Watu wa motoni watamzunguka wamwambie: Ewe fulani wa fulani, una nini wewe? Kwani wewe hukuwa ukiamrisha mema na kukataza maovu? Atawajibu: Naam, lakini mimi nilikuwa nikiamrisha mema, haliyakuwa mimi mwenyewe [nafsi yangu] sitekelezi, na nilikuwa nikikataza maovu haliyakuwa nikiyafanya mimi mwenyewe."*

Hadîth hii ya wazi iliyo swahîh inabainisha na kuashiriya yakwamba miongoni mwa watu ni wale wenye kuwakataza watu wengine mambo, haliyakuwa wao wenyewe wanayafanya mambo hayo. Leo kuna watu wenye kuwakataza watu wengine wajiepushe na Uhizbiyyah, haliyakuwa wao wenyewe wamo ndani ya mahandaki ya Uhizbiyyah, tena wameyang'ata kwa magego yao. Ndugu muheshimiwa- msomaji, haya ni maandiko ambayo Allâh aliyonirahisishia kuyakusanya pamoja, yenye kuonyesha yakwamba si sharuti kuwa mwenye kutahadharisha watu dhidi ya Tahazzub na Hizbiyyah yakwamba yeye mwenyewe awe amesalimika nao na kwamba hatotumbukia kwenye Uhizbiyyah kattu, Laa. Naapa kwa yule ambaye roho yangu iko kwenye mikono yake, mimi nimewahi kuona, kama walivyowahi kuona wengine, kifusi cha muozo wa Uhizbiyyah kwa watu fulani ambao ni wakali kabisa dhidi ya Uhizbiyyah wa watu

wengine, kama vile wanaposema, **"kama wewe huko pamoja na sisi, basi wewe ni dhidi yetu"**. Tafauti iliyoko baina ya Manhaj ya Salafi na mapote ya kuchukiza imejificha kwao. Jambo lenye kuharibu suala hilo zaidi ni kwamba wao ni watu wa pote kwa jina la Salafiyyah, wenye kuwakosea heshima ma-'Ulamâ', wenye kuwavunjia heshima wanafunzi wa 'Ilmu, wakijinyanyua daraja zao juu ya Waislamu, wakijishangaa wenyewe kwa rai zao na kukataa kila naswiha wanazopewa. Sheikh wetu, al-'Allâmah Muhammad Bin Sâlih al-'Uthaymîn (رحمه الله) alibainisha ukweli wa Uhizbiyyah pindi alipoulizwa, na inapatikana katika *Liqâ' al-Bâb al-Maftûh (No.57):*

Twamuomba Allâh akuzidishie katika wema! Sisi twataka kujua ni nini Salafiyyah? Na jee, twafaa kujinasibisha nayo (hiyo Salafiyyah)? Jee, twafaa kuwalaumu wale ambao hawakujinasibisha nayo? Au twafaa kulaumu jina 'Salafi' au jina jengine lisilokuwa hilo?

Jawabu kutoka kwa Imâm 'Uthaymîn:

Salafiyyah ni kufuata njia ya Mtume (ﷺ) na Maswahaba zake, kwani wao ndiwo Salaf wetu waliotutangulia, kwahiyo kuwafuata wao ndio Salafiyyah. Ama kuchukulia Salafiyyah kuwa ni Manhaj (mfumo) maalum, kiasi cha kwamba kila anayekwenda kinyume nayo anazingatiwa kuwa mpotofu hata kama yuko kwenye msimamo wa haki (yaani; Juu ya Salafiyyah); basi hapana shaka huo ni msimamo ulio kinyume cha Salafiyyah. Salaf wote wanalingania kwenye Uislamu na kushikamana juu ya Sunnah za Mtume (ﷺ), na wao hawakumtangaza kuwa ni mpotofu mtu yoyote mwenye kutafautiana na wao (katika mas'ala fulani) kwa sababu ya (kutafautiana) katika tafsiri (Ta'wîl) isipokuwa katika mas'ala yanayohusiana na 'Aqîdah kwa sababu wanamzingatia yule ambaye ana 'Aqîdah tafauti kuwa ni mpotofu.

Lakini katika zama zetu hizi, baadhi ya watu waliochukuwa njia ya Salafiyyah humzingatia kuwa mpotofu kila ambaye anayetafautiana nao hata kama haki itakuwa kwenye upande wa yule anayezingatiwa kuwa mpotofu. Na wakachukuwa Manhaj ya ki-Hizbi, kama walivyochukuwa upande ma-Hizbi wengine walioigawanya Dini na kuwa mapote. Njia hii (yao) haina budi ikataliwe mbali na wala isikubaliwe. Husemwa, "Angalia njia ya Salaf as-Sâlih na yale waliyoyafanya kuhusiana na ikhtilafu na ukunjufu wa nyoyo zao kuhusiana na ikhtilafu katika mas'ala ambamo ijtihâd ilipokuwa na uwezekano wa kuwepo.

(wanatafautiana wenyewe kwa wenyewe) kiasi cha kwamba wanatafautiana kwenye mas'ala makubwa, kwenye mas'ala (madogo) ya 'aqîdah na mas'ala (madogo) ya 'ilmu – kwa mfano, baadhi yao wanapinga yakwamba Mtume (ﷺ) alimuona Mola wake na baadhi nyengine wanathibitisha. Baadhi yao wanasema, 'amali ndizo zitakazopimwa katika siku ya Malipo', haliyakuwa wengine wameshikilia yakwamba 'vitabu vilivyohifadhiwa 'amali ndivyo vitakavyopimwa.' Vilevile wanakhitilafiana katika mas'ala ya Fiqh, Ndoa, mambo ya uwajibikaji, kununua na kuuza; na kadhaalika.

Licha ya yote hayo, hawakutangaziana upotofu baina yao. Kwahiyo, Salafiyyah inayochukuliwa kuwa ni pote maalum (Hizb) lenye hukmu makhsusi, ambalo wafuasi wake humzingatia yoyote mwenye kuhkitilafiana nao kuwa ni mpotofu (ambao wenyewe ni ma-Salafi), basi hawana cha U-salafiyyah watu hao. Lakini Salafiyyah ambayo ni kuwafuata Salaf katika Îmân, misemo, vitendo, njia zao za kukhitilafiana na umoja wao, njia zao za kuhurumiana na kurehemiana, kama alivyosema Mtume (ﷺ): *"Utawaona waumini katika kuoneana kwao huruma na kuonyeshana mapenzi baina yao na kuwa na ukarimu, wanafanana na mwili mmoja, kiasi cha kwamba iwapo sehemu yoyote ya mwili ina maumivu, basi mwili*

wote utakuwa ni wenye kushirikiana katika kukosa usingizi na kuandamana na homa[2]*."* Basi huo ndiwo U-Salafiyyah.

Ndugu muheshimiwa- msomaji, haya ni makala yenye manufaa kwa uwezo wa Allâh kutoka kwa Sheikh Sâlih al-Fawzân (Allâh amuhifadhi), kwani huwenda yakakufaidisha, amesema (Allâh amuhifadhi):

Wanaojinasibisha na da'wah katika zama zetu wamo wale wenye kuwapoteza watu na lengo lao ni kuwapoteza vijana, wao huwazuiya watu kuingia kwenye Dini ya haki, huwagawanya umati wa Waislamu na wakawatumbukiza kwenye matata. Mfano si katika kujinasibisha au katika yenye kudhihirika, bali mfano ni katika ukweli na matokeo yake ya mwisho. Wenye kujinasibisha na Da'wah wanahitajika wachunguzwe kuhusiana na sehemu walizosoma 'ilmu zao, wameichukuwa 'ilmu yao kutoka kwa nani? Wameleleka wapi? 'Aqîdah yao ni ipi? Angalia vitendo vyao na mafungamano yao na watu, (na iulizwe) wamezalisha mazuri gani? Vitendo vyao vimeleta marekebisho gani? Hali zao hazina budi zifanyiwe upekuzi kabla ya watu hawajadanganyika kwa maneno yao na maumbile yao. Hili ni suala ambalo hususan katika zama zetu hizi halina budi kufanywa, ambapo walinganizi kwenye matatizo wamezidi, na Mtume (ﷺ), amewasifu walinganizi kwenye balaa na matatizo kuwa *"ni kutokamana na ngozi zetu, na watazungumza kwa ndimi zetu."*

Kila Sifa njema zinamstahiki Allâh mwanzoni, katika dhahiri na katika siri, na twaomba Swala na Salamu na baraka zimshukie Mtume Muhammad, ahli zake na Maswahaba zake wote.

[2] Hadîth ya an-Nu'mān ibn Basheer (رضي الله عنه) katika Swahîh al-Bukhârî, kitâb ul-Adab kutoka katika kitabu cha *al-Ijābāt al-Muhimmah*, Uk.47-48.